

TAARIFA YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI NA MATIBABU YA MOYO ZITAKAZOTOLEWA NA TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE KWA WANANCHI WA MKOA WA RUVUMA KATIKA HOSPITALI YA RUFEE YA MKOA YA SONGEA TAREHE 23 HADI 28 JULAI, 2018.

- UONGOZI WA MKOA WA RUVUMA UKIONGOZWA NA MHE. MKUU WA MKOA BI. **CHRISTINA MNDEME** UMEANDAA KUTOA HUDUMA ZA UCHUNGUZI NA MATIBABU YA MAGONJWA YA MOYO KWA WANANCHI WA MKOA WA RUVUMA KWA KUSHIRIKIANA NA **TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE** KATIKA HOSPITALI YA RUFEE YA MKOA YA SONGEA.
- HUDUMA HIZI ZITATOLEWA KUANZIA TAREHE 23 HADI TAREHE 28 MWEZI HUU WA SABA, 2018.
- MAGONJWA YA MOYO YAKO KWENYE KUNDI YA MAGONJWA YASIYOYAKUAMBUKIZA. MAGONJWA HAYA YANAATHIRI MOYO NA MISHIPA YAKE. YANAJUMUISHA KUPANDA KWA SHINIKIZO LA DAMU, KUZIBA KWA MISHIPA YA MOYO, MAGONJWA YA KUZALIWA NAYO YA MOYO KWA WATOTO. N.K
- MARA NYINGI DALILI ZA MAGONJWA YA MOYO (kama vile maumivu ya kifua, mapigo ya moyo kwenda mbio, kupumua kwa shida, kuvimba miguu) HAZIJITokezi MAPEMA HADI MOYO UNAPOSIMAMA KUFANYA KAZI KWA GHAFLE AU MTU KUPATA KIHARUSI. HIVYO UCHUNGUZI WA MARA KWA MARA NI MUHIMU.
- PAMOJA NA UCHUNGUZI WA MAGONJWA HAYA YA MOYO UTAKAOFANYIKA, TUNAWASHAURI PIA WAGONJWA AMBAO TAYARI WALIISHAGUNDULIKA KUWA NA UGONJWA WA MOYO KATIKA VITUO MBALIMBALI VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA WAFIKE HOSPITALI YA RUFEE YA MKOA KUPATA MATIBABU.
- WAGONJWA WATAKAOPATA NAFASI WANAWEZA KUFIKA HOSPITALI YA RUFEE KUJISAJILI KUANZIA KESHO TAHERE 18 HADI 22 JULAI KABLA YA KUANZA KUTOA HUDUMA TAREHE 23 HADI 28 JULAI, 2018.

- UTARATIBU WA KUPATA HUDUMA HIZI UTAFUATA UTARATIBU WA SIKU ZOTE WA KUTOA HUDUMA KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA KAMA VILE KUSAJILIWA MAPOKEZI, KUFANYIWA VIPIMO NA UCHANGIAJI. AIDHA, WAGONJWA WENYE BIMA YA AFYA WANASHAURIWA KUJA NA KADI ZAO.
- ILI KUFANIKISHA UTOAJI WA HUDUMA HII, WATAKUWEPO WAHUDUMU WA AFYA WENYE NEMBO ILIYOANDIKWA **"NIULIZE MIMI"** KUWAELEKEZA WANANCHI KUHUSU UTARATIBU WA KUPATA HUDUMA KWA URAHISI.

IMETOLEWA NA MGANGA MKUU WA MKOA

DKT. GOZIBERT MUTAHYABARWA

SONGEA 17 JULAI, 2018